

# **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**102/1**

## **KISWAHILI INSHA**

**2021**

1. Hii ni insha ya kiuamilifu

Vipengele vya utungo wa aina hii vizingatiwe, yaani muundo na maudhui.

### **a) Muundo**

- i. Anwani ( kutokana na mada)
- ii. Maelezo ya kibinagsi
- iii. Maelezo ya kitaaluma
- iv. Tajriba au uzoefu
- v. Maandishi/ uchapisho
- vi. Uanachama
- vii. Tuzo
- viii. Uraibu
- ix. Wadhamini

### **b) Maudhui**

Hoja za mwanafunzi zilenge taaluma ya utabibu.

2. Mwanafunzi afafanue umuhimu wa maabara katika shule za sekondari

### **Baadhi ya hoja**

- i. Huwezesha wanafunzi kukumbuka maswala waliofunzwa darasani wanapofanya uchunguzi maabarani.
- ii. Huwapa wanafunzi nafasi ya kushuhudia maswala ya kisayansi moja kwa moja.
- iii. Husaidia wanafunzi kuelewa kwa mapana mada zinazofunzwa darasani.
- iv. Hukuza mbinu za udadisi, uchunguzi na uwasilishaji wa matokeo ya uchunguzi.
- v. Wanafunzi hudhihirisha nadharia za kisayansi kutokana na matokeo baada ya uchunguzi.
- vi. Hukuza uwezo wa wanafunzi kutatua matatizo mbalimbali na kufanya maamuzi mwafaka.
- vii. Wanafunzi hupata fursa ya kuelewa uhalisia wa sayansi.
- viii. Hukuza hamu ya wanafunzi kutaka kujua/ kufahamu zaidi kuhusu mada husika.
- ix. Kupata maarifa au stadi za kufanya utafiti katika taaluma nyininge.
- x. Hurekebisha mawazo potovu kuhusu suala fulani.

3. Hii ni insha ya methali.

- i. Kutoa maana na matumizi ya methali.
- ii. Kisa au visa vinavyowiana/ kinachowiana na maelezo ya methali.
- iii. Mtahiniwa aonyeshe namna mtu anapopitia hali fulani mwingine awetayari kupitia hali sawa.

4. Hii ni insha ya mdokezo.

Mtahiniwa atamatishe insha yake kwa maneno yayohayo. Asipotamatisha kwayo atakuwa amepungukiwa kimtindo tu, akadiriwe vilivyo.